

TANGAZO LA SERIKALI Na. 477 la tarehe. 14/6/2024

SHERIA YA UWAKALA WA MELI TANZANIA,
(SURA YA 415)

KANUNI

(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 61(2)(g)(ii))

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA UHAKIKI WA SHEHENA ZA MWAKA 2024

Jina
TS. Na.
386 la 2023

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Uhakiki wa Shehena za Mwaka 2024 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Uhakiki wa Shehena za Mwaka 2023 ambazo hapa zitarejewa kama “Kanuni kuu”.

Marekebisho
ya ya Jedwali
la Pili

2. Kanuni kuu zinarekebishwa katika Jedwali la Pili kwa kufuta namba “8) inayoonekana katika kifungu wezeshi na badala yake kuweka namba “9)”.

Marekebisho ya
Jedwali la Tatu

3. Kanuni kuu zinarekebishwa katika Jedwali la Tatu kwa kufuta rejea ya kanuni ya “9(3)(a)”, inayoonekana katika kifungu wezeshi na badala yake kurejea kanuni ya “8(3)(a)”.

Marekebisho ya
Jedwali la Nne

4. Kanuni kuu zinarekebishwa katika Jedwali la Nne kwa kufuta rejea ya kanuni ya “9(3)(b)”, inayoonekana katika kifungu wezeshi na badala yake kurejea kanunia ya “8(3)(b)”.

*Kanuni Hizi Zitajulikana Kama Kanuni Za Marekebisho ya Kanuni Za Uhakiki
wa Shehena*

Tangazo la Serikali Na.477 (Linaendelea.)

Marekebisho ya
Jedwali la Nane

5. Kanuni kuu zinarekebishwa katika Jedwali la Nane kwa kufuta rejea ya kanuni ya “19(4)”, inayoonekana katika kifungu wezeshi na badala yake kurejea kanunia ya “19(5)”.

Kufutwa kwa
Jedwali la Tisa

6. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kufuta Jedwali la Tisa.

Dodoma,
3 Mei, 2024

MAKAME M. MBARAWA,
Waziri wa Uchukuzi